# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 01-10 JANUARI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini zaidi na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la chini ya wastani. Hali hii ilidhoofisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JANUARI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea uwepo wa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, Kati, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi, na mvua katika maeneo ya ukanda pwani nyanda za juu kaskazini mashariki. Pia vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa viliripotiwa baharini.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini zaidi na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mifumo isababishayo mvua (ITCZ) katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki.

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 JANUARI, 2026.**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz